






# Uchumi na Tozo

## Maoni ya wananchi kuhusu hali ya uchumi wa taifa, na tozo za miamala ya pesa kupitia simu za mkononi

## 1. Utangulizi

Uchumi wa Tanzania umekumbwa na matatizo kadhaa miaka michache iliyopita. Matatizo hayo ni pamoja na matokeo ya janga la Uviko - 19, ambalo limetikisa uchumi wa dunia nzima. Ingawa baadhi ya sekta kama vile sekta ya utalii ziliathiriwa na janga la Uviko-19 na hivyo kupunguza mapato ya nchi, kiujumla Tanzania haikupata matatizo makubwa sana ya kiuchumi kutokana na janga hilo. Vita ya Ukraine iliyoibuka hivi karibuni imesababisha kuongezeka maradufu kwa bei ya mafuta na vyakula duniani kote, huku Tanzania ikiwa haijachukua hatua za kutosha kukabiliana na matokeo hayo hasi.

Pia Tanzania imepata mabadiliko makubwa Badiliko kubwa lililogusa wengi ni kifo cha ghafla na kusikitisha cha Hayati, Rais John Pombe Magufuli kilichopelekea nchi kukabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan kama Rais wa kwanza mwanamke nchini. Ingawa Marais wote wawili wanatoka chama kimoja cha siasa, mitazamo yao kuhusu masuala ya kiuchumi na kisiasa imeonekana kuwa tofauti kwa namna nyingi.

Muhtasari huu unawasilisha takwimu kuhusu uzoefu na maoni ya wananchi wa Tanzania kuhusu hali ya taifa kati ya Oktoba 2021 na Julai 2022. Pia utafiti umejumuisha maoni na uzoefu wa wananchi kuhusu tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu[1] . Je, wananchi

1 Sheria ya Tozo za Miamala ya Simu ya Kutuma na Kupokea kwa njia ya Kielektroniki ya 2021, ilianzisha tozo kwenye miamala ya pesa kwa simu kuanzia Julai 2021. Gharama hizo zilipunguzwa kwa 30% mwezi Septemba 2021 na zikapunguzwa tena mwezi Julai 2022, na hivyo kufanya punguzo la jumla la 60% ya kiwango cha kilichowekwa awali.

Muhtasari huu umeandikwa na kutayarishwa na Twaweza East Africa

15 Mbuyu Circus,
Oysterbay, Karibu na Unicef Tanzania.
P.O. BOX 38342, Dar Es Salaam.

t: +255 22 266 4301 | e: info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

wanaona ni matatizo gani makubwa yanayozikabili kaya zao, na ni masuala gani wangependa kuona Rais anayashughulikia? Je, wanaonaje mambo yanavyoendelea nchini kwa ujumla na kuhusu masuala ya kiuchumi? Je, ni wangapi wanatumia sana huduma za pesa kwa njia ya simu? Wangapi wanaunga mkono tozo za miamala ya pesa kwa njia ya simu? Je, tozo zimeathiri vipi matumizi yao ya huduma za pesa kwa njia ya simu? Na je, wanafahamu na kukubaliana na jinsi Serikali inavyotumia mapato ya tozo hizo kwa shughuli za maendeleo?

Takwimu zilizowasilishwa kwenye ripoti hii zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 3,000 kutoka awamu ya sita (Oktoba na Novemba 2021) na ya saba (Juni na Julai 2022) ya jopo maalum la Sauti za Wananchi. Wahojiwa walichaguliwa kinasibu, na jopo hilo lilikuwa na uwakilishi wa kitaifa. Baadhi ya takwimu hizi zimelinganishwa na takwimu zilizokusanywa awamu zilizopita za tafiti za *Sauti za Wananchi,*[2] zilizofanyika kupitia simu za mkononi, ambapo jopo la wahojiwa walipigiwa simu mara kwa mara kuulizwa maswali ya utafiti juu ya uzoefu na maoni yao kuhusu mada mbalimbali.

Matokeo muhimu ni haya:

- Wananchi wametaja tatizo kubwa zaidi linalosumbua kaya zao ni kupanda kwa gharama za maisha
- Wananchi wanataka serikali za mitaa zielekeze zaidi nguvu zake kuboresha utoaji wa huduma za jamii.
- Vipaumbele vikubwa ambavyo wananchi wangependa Rais avishughulikie ni kupunguza gharama za maisha na kuboresha huduma za afya.
- Japokuwa wananchi wengi zaidi hawana uhakika na mwelekeo wa nchi, wananchi wanaosema nchi iko kwenye mwelekeo sahihi ni wengi kuliko wanaosema haiko kwenye mwelekeo sahihi
- Wananchi kwa kiasi kikubwa wanapendezwa na mabadiliko kwenye huduma za jamii, utawala na usalama katika kipindi cha miezi sita iliyopita, lakini wana wasiwasi kuhusu hali ya uchumi.
- Huduma za pesa kwa njia ya simu zinatumiwa sana na wananchi wengi
- Wananchi wengi wanafahamu kuhusu ongezeko la hivi karibuni la kodi na tozo za huduma za fedha kwa njia ya simu; wengi wao hawaungi mkono mabadiliko hayo. Wananchi wachache ndio wanaofahamu kuhusu kupunguzwa kwa tozo hizo.
- Wananchi wanaripoti kuwa wamepunguza kutuma, kutumia huduma za fedha kwa njia ya simu na pia kiasi cha fedha wanachopokea kupitia simu kimepungua tangu mwezi Julai 2021 (Kwa wakazi wa Dar es Salaam kiasi kimepungua zaidi ya 70%).
- Wananchi hawajui mapato yatokanayo na tozo za miamala ya simu yanatumika vipi

2 Kati ya awamu ya sasa ya ukusanyaji wa takwimu na awamu iliyopita za utafiti kwenye mada zilezile, Twaweza ilifanya jitihada kubwa kuhakikisha inawafikia na kuwahoji watu wale wale waliohojiwa mwanzo. Tulifanikiwa kuwafikia wahojiwa walewale kwa 64% kwa awamu zote mbili za utafiti.


# 2. Mambo 15 kuhusu maoni ya wananchi juu ya hali ya uchumi, na tozo za miamala ya fedha kupitia simu

## Jambo la 1: Wananchi wanasema gharama ya maisha ndiyo tatizo kubwa zaidi linalokabili kaya zao kwa sasa

Karibu nusu ya wananchi wote waliohojiwa (48%) wanataja kupanda kwa gharama za maisha kuwa miongoni mwa matatizo matatu makubwa yanayozikabili kaya zao kuliko masuala mengine. Ikifuatiwa na ukosefu wa ajira na fursa nyingine za kujiingizia kipato (29%), vile vile tatizo la njaa na uhaba wa chakula (26%). Matatizo haya matatu makubwa yanayozikabili kaya nyingi nchini Tanzania yote ni masuala ya kiuchumi.

Haya yanafuatiwa na masuala yanayohusu huduma za jamii, ikiwa ni pamoja na vituo vya afya (23%), maji safi (20%), usafiri (17%) na elimu (15%). Katika masuala hayo yote, idadi ya wananchi wanaotaja huduma za jamii kuwa mojawapo ya matatizo matatu makubwa zaidi yanayozikabili kaya zao imeongezeka katika kipindi cha mwishoni mwa 2020 hadi katikati ya 2022.

**Kielelezo cha 1: Kwa maoni yako, ni matatizo gani makubwa matatu yanayoikabili kaya yako kwa sasa?[3]**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022; **Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000; Na utafiti maalum awamu ya 3 wa (2020) na awamu ya 6 (2021)

3 Jumla ya asilimia zote zinaweza zisifike 100% kutokana na makadirio

Matatizo ya wananchi yanayokabili kaya zao yametofautiana kidogo kwa eneo moja hadi jingine nchini. Kupanda kwa gharama za maisha ni tatizo linalowasumbua sana wakazi wa Dar es Salaam (46%), miji mingine (44%) na wakazi wa vijijini (45%). Hata hivyo, katika maeneo ya vijijini, njaa na uhaba wa chakula (30%) vimetajwa kuwa ni tatizo kubwa linalowakabili zaidi kuliko wakazi wa Dar es Salaam (9%). Vivyo hivyo, tatizo la upatikanaji wa maji safi siyo kubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam (6%) kuliko maeneo mengine (21-22%).

Hata hivyo, wakazi wa Dar es Salaam wanalalamikia zaidi tatizo la ukosefu wa ajira na fursa nyingine za kipato tofauti na wakazi wa maeneo mengine. Pia wanataja kukabiliwa na masuala ya uhalifu na usalama, ingawa matatizo haya ni madogo kwenye maeneo yote.

**Kielelezo cha 2: Kwa maoni yako, ni matatizo gani makubwa yanayoikabili kaya yako kwa sasa?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 2: Wananchi wanataka serikali za mitaa kuelekeza nguvu kwenye kuboresha utoaji wa huduma za jamii

Masuala matatu makubwa yaliyotajwa na wananchi kama vipaumbele vya kufanyiwa kazi na serikali za mitaa yote yanahusu huduma za jamii. Suala la kwanza ni huduma za usafiri, zilizotajwa na karibu nusu (44%) ya wahojiwa wote, zikifuatiwa na vituo vya afya (35%) na upatikanaji wa maji safi (26%). Ubora wa elimu pia umetajwa na wengi kwa 21%. Gharama za maisha zimepanda kwa kasi kiasi cha kuibua wasiwasi kwenye serikali za mitaa, kutoka mwananchi mmoja kati ya kumi (10%) mwishoni mwa 2021 hadi mwananchi mmoja kati ya wanne (24%) hivi karibuni. Wakati huo huo, wasiwasi kuhusu ubora wa elimu na upatikanaji duni wa maji safi umepungua tangu mwishoni mwa 2021.

**Kielelezo cha 3: Vipaumbele gani vikuu vitatu ambavyo ungependa serikali ya mtaa ivishughulikie?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022; **Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 3: Kupanda kwa gharama za maisha na huduma za afya ndio vipaumbele vikubwa ambavyo wananchi wangependa Rais avifanyie kazi.

Nusu ya wananchi (46%) wametaja gharama kubwa za maisha kuwa ni miongoni mwa masuala matatu ya kipaumbele ambayo wangependa Rais ayashughulikie, ikifuatiwa na huduma za afya (42%). Huduma nyingine za jamii pia ziko juu, zikiwemo usafiri (35%) na elimu (28%), pamoja na ukosefu wa nafasi za ajira/kipato (27%).

**Kielelezo cha 4: Ni vipaumbele gani vitatu ambavyo ungependa rais avishughulikie?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

Tukiangazia miaka ya hivi karibuni, wasiwasi wa umma kuhusu usalama wa chakula uliongezeka zaidi mwaka 2017, ikifuatiwa na umaskini na gharama za maisha kwa ujumla. Wasiwasi wa masuala ya kiuchumi umeshuka kidogo mwaka 2021 na 2022 ikilinganishwa na miaka iliyopita, ingawa bado wasiwasi huo juu ikilinganishwa na maswala mengine.

Wasiwasi kwa huduma za jamii umeongezeka sana mwaka 2021 na 2022 ikilinganishwa na 2020. Hii ipo katika huduma za afya, usafiri, elimu na usambazaji wa maji.

Kwa miaka ya hivi karibuni, wasiwasi wa masuala ya kiutawala - hasa ufisadi na usalama - haviko juu sana katika orodha ya vipaumbele vya wananchi. (Japo viliwahi kuwa juu zaidi katika orodha ya wasiwasi kabla ya mwaka 2015)

**Kielelezo cha 5: Kwa maoni yako, ni matatizo gani makubwa yanayoikabili nchi kwa sasa? (/Nini Rais anatakiwa kushughulikia?)**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti maalum awamu ya 7, Jun-Jul 2022 (n=3,000); Sehemu ya 1 Msingi (2012), r10 (2013), r24 (2014), panel 2 r1 (2015), r18 (2017), r26 (2018), r32 (2019); Utafiti maalum r3 (2020) na r6 (2021)

## Jambo la 4: Wananchi wasema nchi inaelekea kwenye uelekeo sahihi, japokuwa wengi hawana uhakika

Asilimia 30 ya wananchi wanasema kwa ujumla nchi ina mwelekeo sahihi kuliko mwelekeo usio sahihi (25%), ingawa wengi zaidi hawana uhakika (44%). Wale ambao hawana uhakika wamepungua tangu mwishoni mwa 2021 (66%). Wakati huo huo, kumekuwa na ongezeko la wale wanaoona mwelekeo wa nchi kuwa mzuri (kutoka 18% hadi 30%) na kuongezeka kwa wale wanaoona mwelekeo usio sahihi (kutoka 16% hadi 25%).


**Kielelezo cha 6: Kwa maoni yako, mambo yanaendaje kwa ujumla nchini Tanzania?**




**Source of data:** *Sauti za Wananchi,* utafiti maalum awamu ya 7, Juni-Julai 2022, r3 (2020) na r6 (2021);
**Msingi:** Wahojiwa wote, n=3,000;
na *Afrobarometer* awamu ya 5 (2012), r6 (2014), r7 (2017) na r8 (2021**)**

Kuna tofauti ndogo ya mtazamo kati ya makundi ya watu kuhusu mwelekeo wa jumla wa nchi. Kutokuwa na uhakika kunabaki kuwa mtazamo mkubwa. Wakati wananchi wenye umri mkubwa wanasema nchi kwenye mwelekeo mzuri, wakazi wengi wa Dar es Salaam wanaona nchi haina mwelekeo mzuri.


**Kielelezo cha 7: Kwa maoni yako, mambo yanaendaje kwa ujumla nchini Tanzania**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

Kuimarika kwa uchumi ni sababu kuu inayotajwa na wananchi wanaosema nchi ina mwelekeo sahihi wakati ongezeko la bei na wasiwasi wa kiuchumi ni sababu inayotajwa na wananchi wanaosema nchi ina mwelekeo usio sahihi.

**Kielelezo cha 8: Kwa nini unasema nchi inaelekea uelekeo sahihi/ usio sahihi?**
*(majibu mengi yanaruhusiwa)*





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 5: Wananchi wana mtazamo chanya kuhusu mabadiliko katika huduma za jamii, utawala na usalama katika kipindi cha miezi sita iliyopita, lakini wana wasiwasi na hali ya uchumi

Wananchi wengi wanasema wameona maboresho kwenye huduma za jamii katika kipindi cha miezi sita iliyopita, hasa katika elimu (68%). Wengi pia wanasema uhuru wa kujieleza (60%), uhuru wa kisiasa (56%), na usalama (59%) vimeimarika.

Hata hivyo, idadi kubwa ya wananchi (68%) wanasema gharama za maisha zimekuwa juu zaidi katika kipindi hicho, na upatikanaji wa fursa za ajira na kipato zimezidi kuwa mbaya (48%) badala ya kuboreshwa (22%)

**Kielelezo cha 9: Kipindi cha miezi sita iliyopita, je, yafuatayo yameimarishwa, yameharibika zaidi au kubaki vilevile?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

Ikilinganishwa na mwishoni mwa mwaka 2021, wakati maswali kama hayo yalipoulizwa kwa wananchi, wananchi sasa wana maoni chanya kuhusu mwelekeo wa maendeleo kuliko hapo awali. Hii inaonekana hasa katika elimu na huduma za afya, pamoja na masuala ya utawala na usalama.

Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka 2021, wananchi tayari walikuwa na wasiwasi wa kushuka kwa uchumi na kuongezeka kwa ukosefu wa ajira. Wasiwasi huu bado upo tangu wakati huo.

**Kielelezo cha 10: Kipindi cha miezi sita iliyopita, je, yafuatayo yameimarishwa, yameharibika zaidi au yamebaki vilevile?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 6: Wananchi wana mtazamo chanya kuhusu hali ya huduma za jamii na masuala ya kiutawala kuliko ilivyo kwenye hali ya uchumi

Katika masuala mbalimbali ya huduma za jamii na utawala, wananchi wana uwezekano mkubwa wa kusema mambo ni mazuri kuliko mabaya katika eneo wanaloishi.

Hata hivyo, linapokuja suala la uchumi, wananchi hawana mtazamo chanya. Wananchi wengi wanasema hali ya uchumi ni mbaya (41%) kuliko wanaosema ni nzuri (9%). Vile vile, wananchi wanasema hali ya fursa za maisha kwa vijana ni mbaya (45%) badala ya nzuri (12%).


**Kielelezo cha 11: Je, unaionaje hali ya yafuatayo katika eneo unaloishi?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

Hata hivyo, kuna viashiria kwamba wananchi wanaona mabadiliko chanya katika maeneo haya ikilinganishwa na mwishoni mwa mwaka 2021.

**Kielelezo cha 12: Je unaionaje hali ya yafuatayo katika eneo unaloishi?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;


## Jambo la 7: Katika kodi, wananchi wengi wana mitazamo inayokinzana kwa wakati mmoja

Karibu wananchi wote (90%) wanakubaliana na wazo la msingi kwamba kodi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Lakini wengi (75%) wanasema kuwa kodi ni kubwa na watu wanahangaika kuilipa.

Uchambuzi wa kina unaonesha kwamba kuna mkanganyiko wa wazi kabisa kuhusiana na maoni ya wananchi juu ya mfumo wa kodi. Karibu wote (88%) wanasema wangependa kulipa kodi bila shuruti, na wengine (67%) wanasema si vyema kuficha kipato ili kulipa kodi chini ya kipato. Hata hivyo, wananchi wanne kati ya kumi (42%) wanasema wangekwepa kulipa kodi kama wangeweza kufanya hivyo. Asilimia 63 ya wananchi wanasema ni wajibu wa wote kulipa kodi, hata kama huduma ni mbovu, lakini nusu (51%) wanasema kwamba huduma mbovu za jamii zinahalalisha ukwepaji wa kulipa kodi.

Kwa hakika hizi ni kauli tata, inaonesha kwamba wananchi wana mvutano kati ya kufanya jambo sahihi na vishawishi vya kukwepa kulipa kodi.

**Kielelezo cha 13: Je, unakubaliana au unapingana na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 8: Sababu kuu iliyotolewa ya watu kukwepa kodi ni kuwa watu wanahisi viwango vya kodi ni vikubwa mno

Wananchi wanne kati ya kumi (39%) wanasema watu wanakwepa kulipa kodi kwa sababu wanahisi viwango vya kodi ni vikubwa, zaidi ya sababu nyingine yoyote. Sababu nyingine zilizotolewa ni pamoja na dhana ya kwamba hawalipwi mishahara mizuri (20%), kwamba kodi hazitumiki vizuri (15%), au kwamba watu hawajui namna ya kuwasilisha kodi zao (11%).

**Kielelezo cha 14: Kwa nini unafikiri watu wanakwepa/hawataki kulipa kodi?**
*(majibu mengi yanaruhusiwa)*





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 9: Wananchi wanahisi kuna ugumu katika uendeshaji wa biashara, lakini pia serikali inaboresha mazingira ya biashara.

Idadi kubwa ya wananchi (88%) wanakubaliana na maoni kwamba gharama za kuendesha biashara zimeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Idadi karibu sawa na hiyo (80%) pia inakubaliana na maoni kwamba kodi na ushuru vipo juu na ni vikwazo katika ukuaji wa biashara.

Hata hivyo, wananchi wengi pia wanakubali kwamba mazingira ya sasa ya kisiasa ya nchi (73%) na hali ya kiuchumi (63%) ni nzuri kwa biashara. Wengi pia wanakubali kwamba serikali inatengeneza fursa kwa biashara ndogo ndogo (72%) na kwamba sasa kuna fursa nyingi za biashara kuliko ilivyokuwa mwaka uliopita (67%).

**Kielelezo cha 15: Je, unakubaliana au kupingana na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 10: Huduma za fedha kwa njia ya simu zinatumiwa sana na wananchi

Idadi kubwa ya wananchi (75%) walieleza kuwa walitumia huduma za fedha kwa njia ya simu mwezi uliopita, ambapo nusu (47%) walifanya hivyo wiki iliyopita. Matumizi ya huduma hizo ni makubwa miongoni mwa makundi yote ya watu, lakini matumizi ni madogo kwa wale walio na viwango vya chini vya elimu na wale wanaoishi kwenya kaya zinazotegemea kilimo kama chanzo kikuu cha kipato chao.

**Kielelezo cha 16: Lini ilikuwa ni mara yako ya mwisho kutumia huduma za fedha kwa njia ya simu?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;


## Jambo la 11: Wananchi wengi wanafahamu kuhusu mabadiliko ya hivi karibuni ya kodi na tozo kwenye huduma za fedha kwa njia ya simu; wengi hawaungi mkono mabadiliko hayo

Wananchi wengi wanafahamu kuwa kodi na tozo za huduma za fedha kwa njia ya simu ziliongezwa mwaka 2021 (80%) na zaidi ya nusu wanafahamu kuwa tozo hizo zilipunguzwa baadaye (55%)[4].

4 Sheria ya Tozo za Miamala ya Simu ya Kutuma na Kupokea kwa njia ya Kielektroniki ya 2021, ilianzisha tozo kwenye miamala ya pesa kwa simu kuanzia Julai 2021. Gharama hizo zilipunguzwa kwa 30% mwezi Septemba 2021 na zikapunguzwa tena mwezi Julai 2022, na hivyo kufanya punguzo la jumla la 60% ya kiwango cha kilichowekwa awali.

Wananchi walio wengi hawakubaliani (23%) au hawakubaliani kabisa (34%) na tozo tangu ilipoanzishwa mara ya kwanza. Hata hivyo, walipoulizwa maoni yao kuhusu kupunguzwa kwa kiwango cha tozo, bado wananchi wengi zaidi hawakubaliani (32%) kuliko kukubaliana (18%) na mabadiliko hayo.

**Kielelezo cha 17: Je, unafahamu kuwa kumekuwa na mabadiliko katika ushuru na tozo kwenye huduma za pesa za simu? Je, unakubaliana na mabadiliko kwa kiasi gani?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 12: Wananchi wanaripoti kupunguza matumizi yao ya huduma za fedha kwa njia ya simu tangu Julai 2021

Wananchi wengi wanaripoti kupunguza kutuma fedha kwa njia ya simu tangu Julai 2021 (44%) kuliko wale wanaoripoti kuongeza kutuma fedha kwa njia hiyo (15%). Idadi ya wanaopokea fedha kwa njia ya simu imepungua tangu Julai 2021 (46%) kuliko wale wanaoripoti kupokea zaidi (14%).


Wakazi wengi wa Dar es Salaam wana ripoti kupunguza kutuma/kutumia pesa kupitia huduma za fedha kwa njia ya simu (71%).

Mabadiliko hayo pia yanawiana na yale yaliyoripotiwa na makampuni ya simu. Kwa mfano, Vodacom Tanzania PLC iliripoti kupungua kwa asilimia 4.4 ya idadi ya watumiaji wa huduma ya M-Pesa kati ya Juni 2021 na Juni 2022, na kushuka kwa jumla kwa asilimia 9.2 ya wastani wa mapato kwa kila mtumiaji (ARPU). Jambo hili limesababisha kampuni kulipa ushuru pungufu wa mapato kwa 74% kati ya Aprili na Juni 2022 kuliko kipindi kama hicho mwaka uliopita. Wanazitaja "athari za ushuru kwenye miamala ya utumaji na utoaji wa pesa kwenye simu ya mkononi" kama sababu kuu ya kushuka huku[5].

5 Vodacom Tanzania PLC, Ripoti ya Robo Mwaka, kwa kipindi kinachoisha tarehe 30 Juni, mwaka 2022

Vilevile, awali Serikali ilitarajia kukusanya TZS 1.254 trilioni kutoka kwenye tozo ya simu[6]. Lakini, hadi mwishoni mwa mwaka 2021, serikali ilikusanya shilingi bilioni 360[7].

**Kielelezo cha 18: Je, umebadilisha kiasi unachotuma/kutumia au kupokea pesa kwa njia ya simu tangu Julai 2021?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 13: Wananchi wana mitazamo tofauti zaidi kuhusu tozo ya miamala kwa njia ya simu

Maoni ya wananchi kuhusu tozo za miamala ya pesa kwa njia ya simu yanatofautiana. Wananchi walio wengi wanakubali kwamba tozo hizo ni njia muhimu ya serikali kupata mapato (asilimia 67) na kwamba inahakikisha kuwa kila mtu anachangia maendeleo ya taifa (63%). Hata hivyo, wachache wanakubali kwamba tozo hizo zitapunguza utegemezi kwa wafadhili (46%) au kwamba

6 Majadiliano ya Bunge, Mkutano wa Tatu, Kikao cha Hamsini na Saba, tarehe 23 Juni, 2021 https://www.parliament.go.tz/polis/uploads/documents/1629351457-23%20JUNI,%202021.pdf

7 GSMA, *Tanzania Mobile Money Levy Impact Analysis* uk. 13 https://www.gsma.com/publicpolicy/wpcontent/uploads/2021/12/spec_tanzania_mm_report_02_22-1.pdf


kodi kwenye miamala ya pesa kupitia simu ni jambo zuri (43%).

Wananchi wanaonesha dalili kwamba wangeunga mkono zaidi tozo hizo iwapo wangekuwa na taarifa kamili za namna mapato yanayopatikana yanavyotumika. Wengi (63%) wanasema wangekuwa tayari zaidi kulipa ushuru kama wangefuatilia jinsi fedha zinavyotumika. Wachache wanasema wanajua jinsi fedha hizo zinavyotumika (39%) au wanaweza kujua kwa urahisi kutoka serikalini matumizi ya fedha zilizokusanywa (44%).

Walio wengi pia walikubaliana na pendekezo kwamba tozo yenyewe siyo tatizo bali gharama za miamala zinazotozwa na watoa huduma (66%) na kwamba tozo hiyo inapaswa kutumika tu kwa miamala mikubwa (52%).

Miongoni mwa wale wanaokubali kwamba tozo hiyo ni njia muhimu ya kuongeza mapato kwa serikali wanasema viwango vya kodi hiyo ni kubwa (26%) kuliko wale ambao hawakubali (11%).

**Kielelezo cha 19: Je, unakubaliana au kupingana na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 14: Wananchi hawana uhakika kuhusu matumizi ya mapato yatokanayo na tozo

Wananchi wengi wanasema hawajui (42%) mapato ya tozo yanatumikaje kuliko wanaosema wanajua (38%). Miradi inayotajwa zaidi ni elimu (26%), huduma za afya (25%), na miundombinu ya barabara (21%).


**Kielelezo cha 20: Serikali imesema kuwa mapato yanayotokana na tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu zinaelekezwa kwenye miradi kadhaa ya maendeleo. Je, ni miradi gani unayoifahamu imetekelezwa kupitia tozo hizo?**
*(majibu mengi yanaruhusiwa)*




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

Wananchi wengi (64%) wameridhishwa na matumizi ya mapato yatokanayo na miamala ya fedha kwa njia ya simu.

**Kielelezo cha 21: Kwa kiasi gani umeridhishwa na jinsi tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu zinavyotumika?**
*(Wahojiwa wote, baada ya kuelezwa ni wapi serikali imeelekeza matumizi ya tozo zinazokusanywa )*





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

## Jambo la 15: Wananchi wametaja maeneo mbalimbali ambayo wangependa kuona tozo za miamala zikitumika

Wananchi wangependa kuona mapato ya tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu za mikononi yakielekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo lakini kipaumbele kikiwa huduma za jamii; huduma za afya (57%), elimu (50%), ikifuatiwa na ujenzi wa barabara (38%), huduma za maji (33%), umeme (20%), kilimo (18%) na mikopo (17%).

**Kielelezo cha 22: Miradi/maeneo gani ambayo ungependa tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu zitumike/zielekezwe?**

*(majibu mengi yanaruhusiwa)*




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti maalum wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 7, Juni-Julai 2022;
**Msingi:** wahojiwa wote, n=3,000;

# 3.Hitimisho

Muhtasari huu unazungumzia mada kuu mbili. Ya kwanza ni hali ya taifa katikati ya mwaka 2022. Ya pili ni maoni ya wananchi kuhusu tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu iliyoanzishwa Julai 2021.

Kwa mwelekeo wa jumla wa nchi, matokeo mawili yameonekana. Kwanza, wananchi wana wasiwasi kuhusu hali ya uchumi wao, hasa gharama za maisha. Hili ndilo linaloongoza katika orodha ya matatizo yanayozikabili kaya na yale ambayo wananchi wangependa Rais ayashughulikie.

Pili, wananchi wanaendelea kutokuwa na uhakika kuhusu mwelekeo wa nchi kwa jumla kwa wakati huu, ingawa hii inaanza kujitatua yenyewe. Mabadiliko ya ghafla na yasiyotarajiwa kutoka Rais mmoja hadi mwingine yalisababisha hali kubwa ya sintofahamu miongoni mwa wananchi kwa mujibu wa takwimu za mwishoni mwa mwaka 2021. Japokuwa idadi kubwa ya wananchi wanaonesha kutokuwa na uhakika, idadi ya wale wanaosema nchi ina mwelekeo sahihi au ambao sio sahihi imeongezeka na kuashiria kupungua kwa hisia za sintofahamu kwa wananchi.

Kwenye tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu, uelewa wa wananchi juu ya suala hilo ni mkubwa, lakini punguzo za kiwango cha tozo liliofanyika mara mbili (Septemba 2021 na Juni 2022) hazifahamiki miongoni mwa wananchi ikilinganishwa na ufahamu wao kuhusu kuanzishwa kwa tozo hizo. La kushangaza zaidi ni jinsi maoni ya wananchi juu ya tozo yanavyotofautiana. Wengi hawakubaliani na tozo hizo kwa ujumla, lakini wengi wao pia wanasema ni chanzo muhimu cha mapato kwa serikali.

Mkanganyiko huu unaoonekana si wa kawaida linapokuja suala la maoni ya wananchi kuhusu masuala ya kodi. Idadi kubwa ya wananchi wanadai kwamba wangelipa kodi bila kushurutishwa. Lakini wananchi hao hao wanasema kwamba wangekwepa kodi kama wangeweza. Mitazamo hii inakinzana. Kuna mvutano ndani yetu: sote tunataka kodi zilipwe ili serikali iboreshe miundombinu na kutoa huduma za jamii, lakini pia sote tunahisi maumivu kwenye kulipa kodi. Mvutano huo huo huenda ukawa msingi wa maoni tofauti kuhusu kodi za miamala ya fedha kwa njia ya simu.

Hoja ya mwisho juu ya kodi  inafaa kuangaziwa. Wananchi wengi wanasema wangeunga mkono zaidi tozo hizo iwapo wangekwa na taarifa kamili ya jinsi mapato yatokanayo na kodi hizo yanavyotumika. Wengi pia wanasema hawajui jinsi mapato yanavyotumika, na wachache wanasema wangeweza kujua endapo wangetaka. Wananchi pia wana mawazo ya namna gani wangependa kuona mapato hayo yanatumika.

Kihistoria, uhusiano kati ya kodi na uwajibikaji wa serikali kwa walipa kodi umekuwa dhaifu nchini Tanzania. Je, kodi ya miamala ya fedha kwa njia ya simu inaweza kuuimarisha? Kwa

kuwa wananchi wengi wanatumia huduma za fedha kwa njia ya simu, tozo hiyo tayari inaongeza mapato kutoka kwa wananchi wengi zaidi. Wananchi wanaathirika moja kwa moja na kodi kwa kila muamala wanaoufanya kupitia simu ya mkononi. Sauti za wananchi hawa zinatuambia kwamba wanataka kujua jinsi fedha zao walizozipata kwa juhudi zao zinavyotumika na wanakabiliwa na changamoto ambazo wanatarajia zitatatuliwa na serikali yao, kupitia mapato hayo. Uwazi zaidi wa matumizi na ushiriki mkubwa wa wananchi katika maamuzi ya mgao unaweza kusaidia kuimarisha uungaji mkono wa wananchi kwa juhudi endelevu za serikali katika kuongeza mapato. Hivyo uwazi na ushirikishwaji ndio kiunganishi cha ubia kati ya wananchi na serikali.